# Uhuru, Haki na Maendeleo ya Watu

CHAMA CHA DEMOKRASIA NA MAENDELEO

CHADEMA



# Ugatuaji wa Madaraka

Serikali ya Chadema itagatua madaraka kwa kushusha mamlaka kamili kwa serikali za Majimbo/Kanda , Mitaa, Vijiji na Vitongoji ili kuzipa uwezo wa kufanya maamuzi kamili katika kutumia fursa za maendeleo zinazopatikana katika maeneo mahalia.



# Kujenga na kumiliki uchumi imara na shirikishi

Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itahakikisha kila Mtanzania anatumia rasilimali za nchi, fursa zilizopo, na vipaji vyake katika kuinua kipato chake na pato la taifa kwa ujumla.



# Kupandisha Madaraja na Mishahara ya Wafanyakazi

Serikali ya Chadema itapeleka bajeti ya nyongeza Bungeni katika mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya kuongeza mishahara ya watumishi wote wa umma, kulipa malimbikizo; sambamba na kuwapandisha maadaraja watumishi wenye sifa na kulipa mishahara inayoendelea na madaraja yao.



# Maazingira Bora ya Uwekezaji

Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi inalenga kufanya mazingira ya uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje kuwa rafiki na wazeshi kwa kupunguza urasimu, utitiri wa tozo na kodi zinazopelekea kufungwa kwa biashara, kuzorota kwa shughuli za uwekezaji na kuporomoka kwa uchumi wa Taifa.

# Katiba ya Wananchi

Serikali Chadema itarejesha upya mchakato wa Katiba ya wananchi kama ilivyokuwa imewasilishwa na Tume ya Jaji Warioba. Aidha Serikali ya Chadema itahakikisha kwamba nchi inaongozwa kwa mujibu wa Katiba na Sheria zinazozingatia misingi ya utawala bora na haki za binadamu.



## Uhuru wa Vyombo vya Habari

Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itahakikisha uhuru wa Wanahabari na vyombo vya habari unalindwa kisheria kwa kuzifanyia mabadiliko sheria zote zinazohusiana na masuala ya habari.






Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi inalenga kuifanya elimu kuwa bora na bure kwa ngazi zote ilikumfanya kila mtanzania anayestahili kupata elimu kuipata bila kikwazo chochote ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu nchini. Aidha kwa wanafunzi wa vyuo vikuu , Bodi ya mikopo utawekwa utaratibu kuhakikisha kuwa wanufaika wa mikopo watarejesha mikopo kwa kipindi cha miaka 25 tangu watakapopata ajira na kiwango cha marejesho hakitazidi asilimia 3 ya mshahara wake na hakutakuwa na tozo au faini .

## Afya Bure kwa Wajawazito, Walemavu, Watoto na Wazee.

Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi inalenga kuwekeza katika kuboresha huduma za afya kwa kuongeza ajira za watumishi katika sekta ya afya kuboresha miundombinu na vifaa tiba. Aidha itahakikisha akina Mama wajawazito, Watoto, Walemavu na Wazee wanapewa kipaumbele cha kwanza katika huduma za afya.



# Kujenga na kumiliki uchumi imara na shirikishi

Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi inalenga kuufanya uchumi kuwa jumuishi na shirikishi kwa kutumia rasilimali za nchi bila kuathiri uhuru wa Taifa. Aidha Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itaimarisha uchumi wa soko utakaoheshimu na kulinda mali za watu, haki ya mitaji katika uwekezaji, biashara huru bila kupoka mamlaka ya umma katika maeneo ya ukusanyaji tozo na kodi.



# Fursa za Ajira na Ujira Bora kwa Vijana

Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi inalenga kufungua fursa za ajira kwa Vijana kwa boresha mazingira ya ujasiriamali, uwekezaji wa ndani katika sekta za kilimo, uvuvi, ufugaji, madini, ujenzi wa viwanda vya kimkakati, michezo, uchukuzi, Sanaa, burudani na utuoaji wa mikopo isiokuwa na masharti magumu.



# Fursa za Kupata Maji Safi na Salama kwa Kila Mtanzania

Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itahakikisha kila mtanzania anapata huduma ya maji safi na salama. Aidha itazifanya mamlaka za maji kuwa nyenzo ya usamabazaji wa huduma za maji safi na salama kwa gharama nafuu.



# Umiliki na Matumizi ya Ardhi

Serikali ya Chadema inalenga kumaliza migogoro ya ardhi inayoendelea kuibuka mara kwa mara baina ya wananchi, mamlaka kwa mamlaka, Wananchi na mamlaka  za hifadhi, migogoro ya wafugaji na wakulima pamoja na migogoro kati ya wananchi na wawekezaji kwa kuanzisha mpango rasmi wa umilikishaji ardhi kwa kila mwananchi na taasisi mbalimbali.




# Kuboresha Miundombinu na Maendeleo Vijijini

Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi inalenga kuboresha miundombinu yote kwa kuiunganisha na maeneo ya uzalishaji mali na masoko ya mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi ili kukuza uwekezaji vijijini na kuongeza pato la Taifa.



# Miundombinu: Uchukuzi, Mawasiliano na TEHAMA

Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi inalenga kuboresha miundombinu ya TEHAMA ili kuwezesha nchi kuingia katika uchumi wa kidigitali na kupanua soko la ajira na mitaji kupitia uchumi wa kimtandao.




# Mali Asilia na Utalii

Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi inalenga kuboresha matumizi sahihi ya mali asili kwa kuhifadhi, kutumia kwa usahihi na kuendeleza mali asili za Taifa. Aidha Serekali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itawezesha ujenzi wa miundombinu ya kisasa kama vile hoteli za kisasa na usafiri kufika katika maeneo husika.




# Michezo, Sanaa na Utamaduni Kibiashara

Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi inalenga kuboresha Michezo, Sanaa na Utamaduni kwa kujenga jengo maalumu la Sanaa za maonesho na maigizo (arena), viwanja vya michezo, shule za michezo, vyuo vya Sanaa na michezo ili kukuza maarifa na ujuzi katika michezo, Sanaa na utamaduni ili kuwa ya kibiashara.



## Kujenga Kilimo, Uvuvi na Ufugaji

Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi inalenga kufanya shughuli za kilimo, uvuvi na ufugaji kuwa za kibiashara kwa kuwezesha Wakulima, Wavuvi na Wafugaji kupata masoko yenye tija ndani na nje nchi.



## Ulinzi na Usalama

Serikali ya Chadema itahakikisha kuwa vyombo vya ulinzi na usalama vinakuwa na zana za kisasa na zinazoendana na wakati. Aidha vitapewa bajeti ya kutosheleza na kwa wakati, kwa ajili ya mavazi, teknolojia na marupurupu mbalimbali, tutaanzisha Bima maalum ya afya kwa watumishi wa vyombo vyote vya ulinzi na usalama wawapo kazini na hata baada ya kustaafu
(Jeshi la akiba)